JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

612 **URAIA**

Muda: Saa 3. **Year: 2024**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja sifa nne za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

2. Ainisha kazi nne za Bunge katika kutekeleza majukumu yake.

3. Bainisha mambo manne yanayoweza kumtofautisha raia wa kigeni na Mtanzania.

4. Bainisha changamoto nne zinazowakabili wakulima katika shughuli zao.

5. Eleza kwa ufupi hoja nne juu ya faida za utandawazi kiuchumi.

6. Eleza kwa ufupi tofauti nne zilizopo kati ya stadi ya mawasiliano aliyonayo Sakala na stadi ya udadisi na ubunifu aliyonayo Muli.

7. Taja mila nne zinazoweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI.

8. Tumia mifano miwili kwa kila kundi kufafanua makundi mawili ya zana za kufundishia na kujifunzia.

9. Toa hoja nne kuthibitisha kuwa ili kuandaa azimio bora la kazi kwa somo la Uraia, mwalimu anapaswa kufanya uchambuzi wa muhtasari.

10. Eleza kwa ufupi aina nne za uraia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Eleza sifa kuu tano zitakazomwezesha mwalimu kuchagua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia.

12. Eleza faida tano za matokeo ya upimaji kwa mwalimu.

13. Eleza manufaa matano ya kutumia mbinu shirikishi ya maswali na majibu katika ufundishaji na ujifunzaji.

14. Thibitisha kwa hoja tano umuhimu wa kiongozi cha Mwalimu kama mwongozo unaomwezesha mwalimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.